



## TAARIFA KWA UMMA Namna ya Kuwasilisha Malalamiko yako LATRA

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) inapokea malalamiko ya wateja kuhusu huduma zinazotolewa na Mamlaka. Malalamiko hayo ni yale yanayohusu vitendo vya rushwa, unyanyasaji, ubaguzi au kutotendewa haki kwa namna yoyote.

2. Endapo una malalamiko au maoni yoyote, tafadhali wasiliana nasi kwa barua pepe [malalamiko@latra.go.tz](mailto:malalamiko@latra.go.tz) au kupitia sanduku la maoni linalopatikana kwenye ofisi za mikoa yote Tanzania Bara.

Pia, unaweza kuwasilisha malalamiko yako kwa njia zifuatazo:

- ✓ Piga simu kwenda Nambari + 255 734 22 00 00
- ✓ Tuma ujumbe mfupi (sms au WhatsApp): +255 734 220 000
- ✓ Au tuandikie kwa anwani ifuatayo:

Afisa Malalamiko, Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), S.L.P 3093, Dar es Salaam, Tanzania

3. LATRA itashughulikia malalamiko yako na kukupa mrejesho mapema iwezekanavyo.

Kwa taarifa zaidi tafadhali tembelea tovuti yetu [www.latra.go.tz](http://www.latra.go.tz)

Imetolewa na;

Mkurugenzi Mkuu,

**Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini**

21 Februari, 2022